MSc Environment and Sustainable Development | OVERDUE Learning Alliance 2022-23

KUWAJALI WANAOJALI: Sera na mikakati ya hatua mbalimbali ya uboreshaji wa vyoo na usafi wa mazingira inayozingatia jinsia

Waandishi
Reham Alotaibi
Daniella Calle-Donado
Abi Chapman
Annabel Collinson
Daniela Diaz
Marisol Esquivel
Shann Goh
Sanjoli Johana Shah

Kuendeleza uboreshaji wa vyoo na usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali ya Mwanza



Kielelezo cha 1: Sheria ndogo za jumuiya zilizochorwa kwenye miamba pembezoni mwa ziwa Victoria, Kigoto, Mwanza, 2023. Picha: Reham Alotaibi

MUHTASARI WA SERA

Mambo muhimu

- Kanuni na sheria ndogondogo za kijamii zinazohusiana huduma ya vyoo na usafi wa mazingira zinachangia mzigo usio na usawa kwa wanawake na kutengwa na jamii. Ili kuleta mabadiliko yenye tija , ni muhimu kupinga mitazamo na sheria ndogo ndogo zilizopo katika jamii

- 'Umaskini wa Muda Mrefu' – wanawake wanabeba mzigo usio na usawa wa kazi za usafi wa mazingira na wajibu wa kutunza familia, unaozuia uwezo wao wa kuendeleza Maisha yao binafsi na ya kiuchumi.

- Kuzuia visaidizi vya kutengwa, imesaidia katika kukuza ukuaji wa mitandao ya kijamii na mifumo ya kusaidiana, ikilenga wanawake wanaohisi kutengwa na jamiii zao kwa sababu ya ukosefu wa msaada na ushiriki katika shughuli zinazohusiana na uboreshaji wa vyoo na usafi wa mazingira.

- Kukuza uelewa mkubwa kwa Jamii kupitia nafasi za pamoja (kuwakuatanisha pamoja) kunaweza kusaidia kukidhi mahitaji ya usafi wa mazingira ya wanawake, kuboresha ustawi wao, kuhimiza hatua za pamoja na kupunguza mzigo kwa wanawake.

- Kujumuisha sheria ndogo ndogo zinazozingatia jinsia na kubadilisha mitazamo ya a kijamii kunaweza kukuza usawa wa kijinsia, kupunguza mzigo wa kazi za wanawake, kuongeza ushiriki wa jamii, na kukuza mazoea bora ya usafi.

Utangulizi

Muhtasari huu wa sera utaelezea na kuchambua jinsi mitazamo na sheria ndogondogo za kijamii zinavyoathiri maisha ya kila siku ya wanawake katika ngazi ya familia na Jamii, (Trulove, 2011) na muonekano wa namna ya uboreshaji wa vyoo na usafi wa mazingira. Mitazamo ya kijamii na sheria ndogo ndogo zinautofauti na kufanana - ambazo zinajidhihirisha kwa kuwatenga wanawake pamoja na majukumu yao ya kila siku (Vouhé et al., 2021). Mitazamo ya kijamii ni imani na matokeo ya kitamaduni ambayo hudhibiti mila na desturi za usafi wa mazingira, na kuimarisha maoni ya unyanyapaa juu ya usafi wa mazingira (Eaton et al., 2021; Jalali, 2021). Sheria ndogo ndogo katika Jamii ni sheria za kijamii na rasmi zilizoanzishwa ili kudhibiti desturi za watu binafsi na za pamoja (Massay, 2019). Ingawa sheria ndogo ndogo zipo kulinda afya ya mazingira na ustawi wa jamii, hatimaye hazijumuishi (Koonan, 2019). Mitazamo ya kijamii, kwa upande mwingine, huimarisha mizigo inayowekwa kwa wanawake ndani na nje ya familia , pamoja na vizuizi kwa watoa huduma. (E).

Wanawake wengi wanakabiliwa na vikwazo vingi katika huduma ya vyoo na upatikanaji wa maji, ikiwa ni pamoja na usalama, ufikiaji, na masuala ya usafi (Carrard et al., 2022). Changamoto hizi ni pamoja na umbali mrefu wa kwenda kuafuata maji , ukosefu wa njia sahihi za kutupa taulo za kike wakati wa hedhi, kuchangia matumizi ya vyoo, kazi za usafi zisizokuwa na malipo , na kutengwa na huduma za kuunganisha maji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA). Mbali na majukumu yao ya kuwaingizia kipato, wanawake wanakabiliwa na wingi wa kazi ya usafi wa mazingira bila malipo, kutunza watoto na nyumba na kulemewa na majukumu ya kila siku. Kwa hivyo, mizigo hii mikubwa na vikwazo – vinavyowekwa na mitazamo ya kijamii, sheria ndogo ndogo, na mienendo ya utawala ya kijinsia- huathiri ustawi wa kiakili na kiafya kwa wanawake na jamii kwa ujumla (Jabeen, 2014).

1. Muhtasari

Ni muhimu kutambua jukumu muhimu la vyoo sio tu kama muonekano wa nje bali pia kama mfano unaoleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji (ESD Learning Alliance, 2022). Kupitia mchanganuo wa uatafiti wa OVERDUE juu ya uboreshaji wa vyoo na usafi wa mazingira katika maeneo ya mijini Afrika - ni wazi kwamba mwingiliano wa mitazamo ya kijamii na sheria ndogo ndogo zinaathiri utendaji na mikakati kwa wanawake pamoja na jamii zilizotengwa. (ibid).

Mitazamo na sheria hizi, pamoja na upatikanaji, uwezo wa kumudu gharama, na masuala ya usalama yanayohusiana na usafi wa mazingira Mwanza, Tanzania, kwa pamoja huathiri mwelekeo wa maendeleo ya miji yenye haki kijamii na endelevu katika eneo ambalo maendeleo katika usafi wa mazingira yanahusishwa na changamoto za kitamaduni (ibid)

1.1 Mzigo usio sawa wa Kazi ya Utunzaji kwa Wanawake.

Matarajio ya kitamaduni na kisheria yanayohusu majukumu ya usafi wa mazingira katika kaya yanadhihirishwa katika mzigo usio na usawa wa fidia ya muda usio na malipo , kazi na huduma za matunzo isiyo na usawa kwa wanawake na baadae husababisaha athari za kimwili na kiakili. . Licha ya makadirio kwamba, duniani kote, kazi zisizo na malipo kwa wanawake zinajumuisha kati ya 10% na 39% ya Pato la Taifa, hivyo mapato yanayopatikana kwa njia za huduma zitoloewazo na wanawake hayaonekani. ;, kwa sababu hiyo wanawake , hawana uelewa na mara nyingi hawashirirkishwi kabisa katika michakato ya kufanya maamuzi (OVERDUE, 2022). Barani Afrika haswa, wanawake hubeba mzigo mkubwa wa kazi ya utunzaji na malezi bila malipo, wakitumia saa 3.4 zaidi katika kazi ya malezi katika familia bila malipo kuliko wanaume (ILO, 2018). Katika utafiti uliopita uliofanywa nchini Tanzania unaonyesha jinsi mitazamo ya kijamii kijamii ilivyogawa majukumu yasiyobadilika kulingana jinsia yanayoelekeza mgawanyo huu wa kazi na malezi katika ngazi ya familia (OVERDUE, 2022; Van Aelst, 2014; Feinstein, et al., 2010).
Kama inavyoonekana katika Lengo la Umoja wa Mataifa la Maendeleo Endelevu la 5.4, mzigo usio na usawa unaowekwa kwa wanawake kuhusiana na muda usiolipwa, kazi na matunzo ni suala muhimu linalokubaliwa katika ngazi ya kimataifa; hata hivyo, bado kuna hitaji la dharura la kutambua kazi ya matunzo au malezi isiyo na malipo katika juhudi za kushughulikia kukosekana kwa usawa wa kijinsia (UN, 2015). Muhtasari huu wa sera unatumika kama nyenzo ya kujenga upya na kufikiria upya sera jumuishi inayoshughulikia mwitikio wa kijinsia, ikichochewa na sauti zenye ari za wanawake katika makazi ya Kigoto. Matokeo yaliyoainishwa katika muhtasari huu yanalenga kutoa ujuzi muhimu na mapendekezo yanayotekelezeka na kutumika kama sehemu ndogo kwa suala kubwa la usawa na maendeleo endelevu.

Kielelezo cha 1: Wanawake wanaoshiriki katika mijadala ya warsha mtaa wa Kigoto, Mwanza, 2023. Picha: Shann Goh

Maoni ya wanawake, kwenye warsha na wanajamii:

Walipoulizwa wakati wa warsha kama wanahisi kutokuwa salama kutumia choo wakati wa usiku, 11 kati ya 14 waliohudhuria walisema hawakujisikia salama.



1.2 Mbinu ya Utafiti

Katika utafiti huu mbinu Mbinu mbalimbali zilitumika , ikijumuisha utafiti wa kina uliotokana na machapisho na ripoti mbalimbali uliofanywa kwa muda wa miezi mitano kukusanya taarifa muhimu za eneo husika ili kutayarisha ukusanyaji wa taarifa wa majumbani. Kufuatia utafiti wa awali kupitia machapisho na ripoti mbalimbali, mbinu hii ilikuwa ni Mbinu ya msingi ambayo ilijumuisha mambo yafuatayo:

1) Matembezi katika eneo husika: yanayojumuisha uchunguzi wa kimfumo,unaohusisha utaratibu wa utafiti kwa kupiga picha na uchukuaji maelezo, kuandika taarifa za hali ya afya ya mwili, , hali halisi ya maeneo ya vyoo, njia za kupita kufika chooni, changamoto za ufikiaji, na uchunguzi mwingine katika makazi yote.

2) Mahojiano ya mtu mmoja-mmoja yaliyofanywa na wanawake ili kupata taarifa juu ya uzoefu wao, mahitaji, na mitazamo inayohusiana na desturi za usafi wa vyoo na mazingira, mitazamo ya kijamii, na majukumu kulingana na jinsia .

3) Majadiliano ya kikundi yaliandaliwa ili kuwezesha mwingiliano wa kikundi, Kuwepo na mazungumzo ya wazi na kujenga ushirikiano miongoni mwa washiriki, na kuruhusu kubadilishana mawazo, uzoefu wa pamoja, na ujuzi ngazi ya jamii.

4) Uchunguzi wa matumizi ya muda ambao ulitumika kukusanya taarifa za matumuzi ya muda wa siku nzima kwa wanawake ili kuelewa uhusiano wa mitazamo ya kijamii na muda wa kazi na malezi ambayo yanaendeleza mzunguko wa umaskini miongoni mwa wanawake na wasichana katika Jamii .

Sampuli zilizopendekezwa zilitumika kuchagua washiriki kwa mahojiano na mijadala ya vikundi ambapo wanawake kutoka makabila na makundi mbalimbali ya umri walishirikishwa ili kupata mitazamo mbalimbali. Idhini ilipatikana kutoka kwa washiriki wote, kuhakikisha uelewa wao wa malengo na taratibu za utafiti. Usiri na kutokujulikana kwa washiriki kulihakikishwa katika mchakato wote wa utafiti. Watafiti walidumisha usikivu kulingana na mitazamo ya kitamaduni, mila na desturi za mahali hapo ili kuepuka kusababisha madhara au makosa.

Kupitia utafiti wa kina, ujuzi na mapendekezo kwa vitendo yalitayarishwa. Hata hivyo, mipaka ya utafiti huu yazingatiwe wakati wa kuwasilisha matokeo.

Kwa sababu ya uhaba wa rasilimali na ukomo wa muda, ukubwa wa sampuli ya washiriki katika matembezi ndani ya mtaa , mahojiano, na mijadala ya vikundi lengwa ulikuwa mdogo, na uwezekano wa kuathiri uwakilishi wa matokeo. Kwa hivyo, tahadhari inapaswa kuchukuliwa wakati wa kujumuisha matokeo zaidi ya muktadha maalum wa masuuhisho utofauti wa lugha na tamaduni kati ya watafiti na washiriki pia vilileta changamoto katika kuelewa kikamilifu na kutafsiri majibu. Changamoto hizi zinaangazia hitaji kubwa la utafiti na mitazamo mipana zaidi ili kuimarisha uhalali na utekelezaji wa mipango na sera siku zijazo .



Mchoro wa 2: Choo cha Jumuia cha binasi chenye sehemu za kuogea na huduma ya kujisaidia Kigoto, Mwanza, 2023. Picha: Reham Alotaibi


Wasiwasi
Matumaini
Usalama nyakati za usiku
Ugumu wa kupata huduma ya maji
Kutengwa
Upatikanaji wa huduma ya choo
Matatizo ya kiafya
Faragha na hedhi
Ukosefu wa maji muda wote
Usafi
Usalama wa watoto
Uboreshaji wa usalama, afya na ustawi
Ulinzi na uhifadhi wa mazingira
Ushirikiano wa Jumuiya na kufanya kazi pamoja - kuunda
Uhuru wa kifedha na uhuru
Habari, upatikanaji na elimu
Ubora wa maisha ulioboreshwa
Matukio ya kila siku
Sababu kuu
Kukosekana kwa miundombinu
Ukosefu wa msaada thabiti
Ukosefu wa upatikanaji rasilimali
Kutokuwepo kwa jamii

Mchoro wa 3: Mti wa Wasiwasi, Matakwa na Sababu za Msingi. Maswala na matakwa ya usafi wa mazingira ya wanawake yalikusanywa wakati wa mahojiano. Wasiwasi umeainishwa katika sehemu ya juu ya tatu ya kushoto ya mchoro, wakati matakwa yanaelezewa juu ya kulia. Utafiti unaongoza kupata sababu za msingi za maswala yawanawake, yaliyogawanywa katika makundi makuu manne. Hizi zinaweza kupatikana katika theluthi ya chini ya mchoro. Kielelezo: Calle, D., 2023

2. Matokeo & Mapendekezo

Mapendekezo yanalenga kushughulikia sababu za msingi za mizigo isiyo sawa pamoja na matatizo ya kila siku, ili kukidhi matarajio ya wanawake.

2.1 Kituo cha Matunzo

Matokeo:

Baada ya kufanya mahojiano na baadhi ya ,wanawake, wamegundulika kuwajibika zaidi kwa malezi ya watoto na kazi za usafi wa mazingira jijini Mwanza. Wanawake wengi wanawajibika na mswala yote ya usafi wa nyumbani; hii ni pamoja na kusafisha vyoo, kusimamia usafi au kufua nguo. Wanawake wanaoishi kwenye nyumba za kupanga mara nyingi hufanya usafi kwa utaratibu wa zamu, ambazo hufanyika miongoni mwa wapangaji wa kike; Ila kwa familia ambazo hazichangii huduma ya choo wanawake ndio wahusika wakuu katika swala la usafi. Zaidi ya hayo, kuna wanawake wengine hufanya kazi za kuingiza kipatao kwa familia hivyo kuwaacha wakiwa na muda mchache wa kujitunza wenyewe.

Zaidi ya hayo, wanawake walionyesha ugumu wa kufikia na kutumia vyoo (ona Mchoro 3). Makundi yaliyoathirika zaidi ni wazee na walemavu wa mwili, huku baadhi ya wanawake wakielezea kulazimika kutambaa ili kukufikia chooni, au kutokuwa na mwanga wa kutosha kukitumia kumulika nyakati za usiku. Zaidi ya , wengi waliohojiwa waliripoti kuhisi kutokuwa salama kwa kutumia vyoo nyakati za usiku kwa sababu ya hatari ya kuanguka, kukutana na wanyama au kuathiriwa na unyanyasaji wa kimwili au wizi. Kwa hiyo, wanawake wengi wanalazimika kutumia ndoo ndani ya nyumba zao, jambo ambalo husababisha usumbufu na kuleta matatizo ya usafi wa mazingira.

Katika kusimamia hali ya vifaa vyao vya usafi, wanawake hubeba mizigo ya kimwili na kisaikolojia ya kuhakikisha usafi wa mazingira kwa familia zao. Wanawake waliohojiwa walionyesha hisia za upweke, uchovu na wasiwasi wao wenyewe na afya na usalama wa watoto wao.

Utekelezaji wa Kituo cha Huduma:

Kituo cha Huduma kinaweza kutoa mahitaji mbalimbali katika ngazi ya Jamii. Kiuhalisia, ni jukwaa la usafi wa mazingiira ambalo linatoa usalama pamoja na faragha. Hata hivyo, msingi wake, Kituo cha huduma kinatoa majibu ya uhitaji wa jukwaa la pamoja. Ni jukwaa la watoa huduma za usafi wa mazingira na wanajamii kujumuika pamoja, kujadili masuala na kubuni mbinu na nafasi ya kujenga jamii. Kituo cha Huduma ni chaguo la kimkakati la kukuza usitahimilivu wa jamii, kuwawezesha wanajamii na kujenga uwezo wao wa kutatua changamoto za kijamii.

Kwa ushirikiano na wafanyakazi wa eneo la usafi wa mazingira, kwa kuzingatia vipengele vyote muhimu vya Kituo - ikiwa ni pamoja na eneo, muundo, faragha, ufikiaji na usalama - Kituo cha Huduma kinapaswa kutoa huduma safi za usafi wa mazingira na vyoo vya kumwaga maji, nafasi ya kuoga, na eneo la kuosha nguo. Inapaswa kujengwa kwa kwa kutenganisha vyoo vya wanaume, wanawake na watoto; Kituo hicho kinapaswa kuwa katika eneo ambalo linafikiwa kwa urahisi na wanajamii wote, na kuwajumuisha pia watu wenye maalaumu maalumu. Saa za kazi zilizopendekezwa ni kutoka 12 asubuhi hadi 4 za usiku.

- Eneo la choo la watoto lazima lipewe kipaumbele na Kuwepo na namna rafiki ya kufika chooni pamoja na usafi wa choo; Kituo cha huduma kinapaswa kiwe rafiki wa Watoto wanaoweza kutumia choo peke yao na wale wanaohitaji uangalizi wa wazazi au walezi.
- Eneo la wanawake linapaswa kuzingatia ufaragha na usalama, na kutengeneza nafasi ambapo wanawake wanahisi salama na amani. Mambo yanayopaswa kuzingatiwa ni uwepo wa komeo imara, taa, vioo vya kujianagalizia, na ndoo maluumu ya kuweka taulo za hedhi. Kama jambo la ziada, maduka makubwa ya wanawake na wasichana yanaweza kusaidia kuboresha ustareheshaji na ufikiaji, haswa kwa wale walio na shida za mwili au wenye watoto (Schmitt et al., 2018).
- Nafasi za wazee na walemavu zinapaswa kutoa kipaumbele ulemavu wa mwili, ikiwa ni pamoja na vyoo vya kukaa, taa zenye mwanga unaofaa na sehemu za kushika kwa ajiri ya usalaama. (UNICEF, 2023). Kwa msingi wake, Kituo cha huduma ni jukwaa la jamii kubadilishana maarifa:
- Kituo cha taarifa za afya ili kuruhusu maafisa wa afya ya jamii kukutana na jamii na kubadilishana maarifa ya usafi wa mazingira na afya.
- Bodi ya mawasiliano na matangazo yenye lengo la kukuza huduma na kupeana habari.
- Nafasi ya matumizi ya binafsi ili kuwapa wanajamii usalama na nafasi salama ya Jamii ili kujitunza wenyewe kwa uhuru .
- Mahali pakukutania ambapo vikundi vya jamii vinaweza kutumia kuhamasisha mswala ya ujasiriamali na elimu ya fedha au kutayarisha warsha na makongamano ili kukuza ushirikiano na mtandao wa kusaidiana.

Kituo cha huduma kinapaswa kusimamiwa na wanawake, kwa kuwapa nafasi wanawake kuwa wasimamizi wa wakuu wa kituo na kuwahamasisha wanawake kuwa viongozi katika jamii zao (Caruso et al., 2022). Nafasi hii pia inaweza kuruhusu uzalishaji wa mapato, kuongeza uwezo wa kifedha miongoni mwa wanawake na kuwajengea uwezo kwenye jamii zao (Mengistu, 2012). Wanawake waliochaguliwa ndani, kwa ushirikiano na serikali ya mtaa, wanaweza kuhalalisha juhudi hizi na michakato ya usimamizi wa Kituo cha Huduma (Chaplin, 2017). Kupitia elimu na uwezeshaji, Kituo cha Huduma kinaweza kuendeleza usafi wa vyoo na usafi wa mazingira salama, kuruhusu wanawake kujitunza wenyewe na kuhimiza watu ndani ya jamii kusaidiana.
Njia nyingine ambayo Kituo cha Huduma kina uwezo wa kuhimiza na kukuza umuhimu wa kifedha na kukuza ukuaji wa jamii ni kwa kuunda nafasi ambapo watu wanaweza kutoa huduma na bidhaa zao na nafasi ya kujifunza kwa jamii kubadilishana ujuzi na maarifa mbalimbali.

Kama matokeo, uwekezaji unaofanywa katika Kituo hiki utarejeshwa kwa jamii, kupata chanzo cha mapato ambacho kinachangia uhuru wa kifedha wa wanawake, kuwezesha jamii na pia kuhimiza ukuaji wa uchumi.

2.2 Maendeleo ya kaya ya vikundi

Matokeo:

Katika jamii nzima, kuna huduma mbalimbali za usafi wa mazingira, ikiwa ni pamoja na vyoo vilivyoboreshwa, vyoo vya mashimo ya asili, vyoo vya kumwaga maji vya kisasa, na vyoo vya kumwaga maji kwa mikono. vyoo tu kati ya hivi vilivyounganishwa na MWAUWASA. Wanawake katika kaya ambazo hazijaunganishwa na mfumo wa majitaka wanalazimika kutumia muda mwingi katika majukumu ya kila siku ya usafi wa vyoo na mazingira.

Uendelezaji kwa kundi la kaya:

kwa kuzingatia lengo la MWAUWASA la kuongeza kiwango hadi asilimia 100 kwa wakazi ifikapo mwaka 2040, utoaji wa maji kwa pamoja na ufanisi unapaswa kutekelezwa kupitia kuunganisha maji kwa pamoja (Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, 2008). Uunganishaji wa kimakundi unaweza kuboresha utoaji wa maji huku ukisisitiza umuhimu wa ongezeko la kiwango cha Uchumi, ili kutoa uwezo wa kumudu kwa MWAUWASA na familia.

Kukuza huduma ya kuunganishwa maji kwa kundi la kaya badala ya kaya moja moja, kukuweka pointi kuu ya kuungia kutaongeza idadi ya nyumba nyingi kuunganishwa kwenye mtandao wa maji wa MWAUWASA na kupunguza miundombinu isiyo ya lazima.

MWAUWASA na wakazi wanaweza kunufaika na hali ya kiuchumi kwa kuokoa gharama za uwekezaji kuunganisha miundombinu ya maji kwa makundi ya kaya kwa pamoja ambazo zingetumika kwa kuunganisha kila nyumba kivyake. Matokeo yake, zaidi rasilimali zinaweza kuelekezwa katika utunzaji na uboreshaji wa huduma.



Kielelezo cha 4: Kitovu cha Uangalizi. Kimeundwa kusaidia jumuiya kupata mahali pa mikutano na Kupata huduma bora usafi wa mazingira, imeonyeshwa hapo juu. Wanawake wanaweza kutumia muda wao wenyewe wanapotumia huduma ya choo ambacho ni safi na pia wanaweza kushiriki katika matukio ya elimu au vikao vya jumuiya katika Kituo cha cha Jumuia. Kielelezo: Calle, D., 2023.



Kielelezo 5: Uunganishwaji kimakudni. Upatikanaji bora wa maji kwa kaya unawezekana kupitia viunganisho vya makundi. Njia ya sasa ya uunganisho inaonyeshwa upande wa kushoto, wakati chaguo bora la uunganisho kwa wakazi linaonyeshwa upande wa kulia. Kielelezo: Calle, D., 2023.

Utekelezaji-shirikishi unapaswa kutiliwa mkazo katika utekelezaji wa kuunganisha makundi ya maeneo, kuhimiza kamati ya wanawake iliyoteuliwa ndani kuhusika katika mchakato wa kubuni na utekelezaji na kuhakikisha ufanisi wa uwekezaji.

Mikutano ya mara kwa mara ya Jamii inapaswa kuongozwa na kamati ya mtaa, na kutoa nafasi kwa Jamii kuchangia uzoefu wao na maoni juu ya huduma. Mikutano hii inaweza kutumika kama jukwaa la kufanya maamuzi ya pamoja.

2.3 Rasilimali na sauti

Matokeo:
Nchini Tanzania, wanawake, kwa wastani, wafanya kazi masaa 14 kwa siku, kinyume ilivyo kwa wanaume wanaofanya kazi masaa 7 kwa siku (ESD Learning Alliance, 2022). Kulingana na tafiti za matumizi ya muda takriban asilimia 50% ya muda wa wanawake hutumiwa kwenye kazi ya usafi wa mazingira ambazo hazina malipo. Kazi hii isiyonamalipo inapewa uzito na sheria ndogo ndogo na tamaduni ndani ya jamii; sheria hizi ni za kinadharia zisizoegemea upande wa kijinsia lakini, katika utekelezaji, zina athari za kijinsia (Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, 2008). Kwa hivyo, sheria ndogo ndogo zina athari za kijinsia hata kama hazijaonyeshwa wazi.

Zaidi ya hayo, wanawake walio kwenye vikundi vya kuweka akiba vya kijamii walionekana kuwa hali ya matumaini na umoja na kutetea wa kikundi kujengewa uwezo na ufanisi. Wale ambao walionyesha nia ya kuwa sehemu ya kikundi cha akiba mara nyingi hawakuweza kwa sababu ya vikwazo vya kifedha.

Ni wazi kwamba kanuni za kijamii na sheria ndogo ndogo ni kikwazo cha kujitunza mwenyewe, uhuru wa kifedha, upatikanaji wa muda, na umuhimu wa kimatokeo.



Kielelezo cha 6: Rasilimali na Sauti za Wanawake. Katika kusahihisha na kufasiri upya kanuni na miongozo ya kijamii, kufanya maamuzi lazima kujumuishe wanajamii, haswa wanawake na walezi. Kielelezo: Calle, D., 2023.

Mapendekezo yanayojikita katika kujumuisha sheria ndogo ndogo za jumuiya na miongozo ni muhimu. Vikundi vya akiba vya jamii vinavyojipanga vinaweza kukuza uhuru na umuhimu wa kimatokeo ndani ya jamii, na kujenga fursa za maendeleo ya kiuchumi kwa wanawake.

Rasilimali na Utekelezaji wa Sauti:
Sehemu ya kwanza ya mkakati huu inapendekeza vikundi vya akiba vilivyo anzishwa na kuundwa kwa ajili ya wanawake, ambavyo vinaweza kuzalisha mapato kwa mahitaji yanayohusiana na usafi wa mazingira na juhudi za ujenzi wa jamii (Kesanta na Andre, 2015).

- Vikundi vya kuweka akiba vinaweza kusaidia matarajio ya wanawake kutafuta fursa za maendeleo ya kiuchumi na kutumika kama mfumo wa kusaidia jamii; hii itakuza hali uongozi kwa wanawake, kuwezesha hatua za ndani, na kuhimiza maendeleo jumuishi (Rickard, 2022:48).

- SaVikundi vya kuweka akiba vinapaswa kupangwa kulingana na mahitaji ya jamii, na kusisitiza utofauti na ushirikishwaji wa kuzingatia uwezo tofauti wa kifedha wa wanawake. Vikundi vya kuweka akiba lazima vijikite katika ufadhili huku vikizingatia nyanja zote za jamii, kuwapa wanawake zana za kujengea uwezo.
- Msaada na mafunzo lazima yatolewe kwa vikundi vya kuweka akiba ili kuwawezesha kukua. Hii lazima ijumuishe warsha na elimu juu ya maswala ya kifedha.

Pili, ili kufikia sheria ndogo ndogo jumuishi, sauti za wanawake wote bila kujali kabila, umri, dini na tabaka lazima zijumuishwe katika mchakato wa maendeleo (King na Mason, 2001). Kwa sababu hii, sehemu ya pili ya mkakati huu inapendekeza kufanya maamuzi ya pamoja na kubadilishana ujuzi katika ngazi zote za utawala ili kuandaa sera kamili, inayo jumuisha watu wote (Moser, 1993). Ili kufikia haki ya usafi wa mazingira uzoefu mkubwa unapaswa kuzingatiwa, kuangazia umuhimu wa ushirikishwaji wa wanawake katika michakato ya kufanya maamuzi (Rusca, Alda-Vidal, na Kooy, 2018).

- Wanawake katika jamii wanapaswa kujumuishwa katika marekebisho ya sheria ndogondogo, zinazozingatia uzoefu wa wanawake katika miongozo mipya ya kijamii. Kufanya hivyo kutawezesha sheria ndogo ndogo kuakisi kwa usahihi na ipasavyo mahitaji ya wanawake na wasichana katika jamii (Koonan, 2019).

- Jukwaa la Usafi wa Mazingira linapaswa kutoa nafasi kwa watoa huduma, kuruhusu wanawake kutoa maoni yao kuhusu usimamizi wa masuala ya vyoo na majukumu yao muhimu katika kuchangia usafi wa jamii na familia zao.

- Kuhimiza kujenga uwezo katika ngazi zote ni muhimu, ikijumuisha mafunzo kwa wawakilishi wa jamii kuhusu masuala muhimu ya jamii kama vile maendeleo ya uboreshaji vyoo na usafi wa mazingira na upatanishi na mazungumzo. Kazi hii inaweza kusaidia ushirikishwaji wa maarifa na kuhakikisha ufanyaji maamuzi unaofaa..

Kisanduku cha 1:
“Nguvu ya kikundi cha akiba”
Nia ameishi Kigoto kwa miaka 15 na ni mama wa watoto mmoja 6. Anahudumia familia yake kwa kufanya kazi usiku kucha akiuza samaki. Kama ilivyo kwa wanawake wengi wa Kigoto, yeye ndiye anaeingizia kipato familia yake. Pamoja na jukumu lake kama mama pia ana jukumu la kuhakikisha maswala yote yanayohusu choo kwa familia yake. Nia pia ni mwanachama wa kikundi cha kuweka akiba- klichoanzishwa miaka 3 iliyopita. Kwa sasa kikundi kina wanachama 12, na kila mmoja anachangia shilingi 4,000 (TZS) kila wiki. Kikundi hiki kilianzishwa kwa ajili ya wanawake wanaopenda shughuli za kuwaongezea kipato, lakini fedha zinaweza kutumika kwa ajili ya kuboresha usafi wa mazingira na mahitaji ya afya, miongoni mwa wanakikundi. Ndani ya kikundi, wanawake walijenga hali ya kuaminiana na kufarijiana, Hushirikishana maswala yao yote pindi wanapokutana kwenye vikao vyao. Nia pia anakiri kwamba kuwa katika kikundi kulimsaidia kujiamini na kujieleza hadharani. Ingawa kikundi kilianza kama kitu cha hiyari, kimebadilika na kuwa kikundi cha kujaliana kinachoangazia jukumu la vikundi vya jamii..

> ***“Wanawake waliowezeshwa pia wameunganisha shughuli zinazohusiana na maji, usafi wa mazingira na usafi na biashara ndogo ndogo, zinazozalisha mapato muhimu ya kaya kusaidia mahitaji ya kielimu na lishe ya familia zao, na kuthibitisha kuwa uwekezaji katika maji salama na usafi wa mazingira huleta mabadiliko mapana na makubwa zaidi kwa maisha ya wanawake na wasichana kuliko faida rahisi za kiuchumi”.***
>
> **Lydia Zigomo**
> (kama ilivyojatwa kwenye Mengistu, 2012:4)

3. Hitimisho

Kupitia utafiti na uchanganuzi, muhtasari huu wa sera umehitimisha kuwauzoefu wa wanawake uliathiriwa na kubadilishwa kwa utumiaji wa vyoo bora. Kutokuwepo au kuwepo kwa jamii kunaathiri uhusiano kati ya ustawi wa afya wa mwili na kiakili kwa wanawake na usafi wa mazingira. Mitazamo ya ya kijamii, , ilichangia kwa kiasi kikubwa wanawake kuhisi kutengwa katika kazi ya usafi wa vyoo na mazingira

Kwa hiyo, mapendekezo lazima yakazie hitaji la kuwajali wale wanaojali. Mawazo na mapendekezo ndani ya muhtasari huu yanashughulikia mahitaji ya kiutendaji na ya kimkakati ya wanawake, yakisisitiza maswala yao muhimu katika suluhu na kushughulikia mahitaji yao kupitia njia zilizounganishwa, zinazolenga jamii (Mo-ser, 1993). Katika makutano ya suluhu hizi ni jamii yenyewe, ambayo inapaswa kupewa kipaumbele ili kupunguza kutengwa kwa wanawake ili kusaidia hatua za pamoja na maendeleo endelevu.

Usafi wa vyoo na mazingira shirikishi , unaozingatia maswala ya kijinsia haufaidishi wanawake pekee—unawezesha jamii nzima. Utafiti ujao na ushiriki wa jamii unapaswa kubadilika kwa kuondoa uwajibikaji kwa wanawake pekee, kukabiliana na umaskini na mzigo usio na uwiano, na kupunguza hali ya wanawake kutengwa kwa katika jamii

Shukrani

AKama kikundi, tunapenda kutoa shukrani kwa walimu wetu katika Kitengo cha Mipango ya Maendeleo(DPU), Prof. Adriana Allen, Rita Lambert na Pascale Hofmann, kwa usaidizi na mwongozo wao wakati wa shughuli za vitendo nje ya nchi na kwingineko. Pia tunawashukuru sana wawezeshaji wetu nchini Tanzania, Sheila Salum na Dr. Tatu Mtwangi Limbumba. Mwisho , tunatoa shukrani zetu kwa wanawake waliochangia katika utafiti huu, ambao bila wao muhtasari huu wa sera usingewezekana.

Marejeleo

[1] Carrard, N., MacArthur, J., Leahy, C., Soeters, S. & Willetts, J., 2022. ‘The water, sanitation and hygiene gender equality measure (WASH-GEM): Conceptual foundations and domains of change’, Women’s Studies International Forum, 91, 102563.

[2] Caruso, B., Conrad, A., Patrick, M., Owens, A., Kviten, K., Zarella, O., Rogers, H. & Sinharoy, S., 2022. ‘Water, sanitation, and women’s empowerment: A systematic review and qualitative metasynthesis’, PLOS Water, 1.

[3] Chaplin, S., 2017. ‘Gender, urban sanitation inequalities and everyday lives: A literature review and annotated bibliography’. Centre for Policy Research

[4] Eaton, J., Krishna, A., Sudi, C., George, J., Magomba, C., Eckman, A., Houck, F. & Taukobong, H., 2021. ‘Gendered Social Norms Change in Water Governance Structures Through Community Facilitation: Evaluation of the UPWARD Intervention in Tanzania’, Frontiers in Sociology, 6, 672989.

[5] ESD Learning Alliance, 2022. Work not duty. Video produced as group output for the Learning Alliance between OVERDUE and MSc Environment and Sustainable Practice Module at the Bartlett Development Planning Unit, University College London. [Online] Available at: https://www.youtube.com/watch?v=wlJKntciRX0 [Accessed 17 May 2023].

[6] Feinstein, S., Feinstein, R., Sabrow, S., & Feinstein, S., 2010. Gender Inequality in the Division of Household Labour in Tanzania. African sociological review. 14(2), 98–109.

[7] ILO, 2018. ILO calls for urgent action to prevent looming global care crisis. [Online] Available at: https://www.ilo.org/africa/media-centre/pr/WCMS_633460/lang--en/index.htm#:~:text=In%20Africa%2C%20women%20spend%203.4,paid%20work%20are%20added%20together. [Accessed 19 May 2023].

[8] Jalali, R., 2021. ‘The Role of Water, Sanitation, Hygiene, and Gender Norms on Women’s Health: A Conceptual Framework’, Gendered Perspectives on International Development, 1, 21–44.

[9] Kesanta, J. & Andre, B., 2015. ‘Impact of Women Empowered through Community Savings Groups on the Wellbeing of their Families: A Study from Mgubwe, Tanzania’, Interdisciplinary Journal of Best Practices in Global Development, 1.

[10] King, E. & Mason, A., 2001. Engendering Development: Through Gender Equality in Rights, Resources, and Voice, The World Bank.

[11] Koonan, S., 2019. ‘Sanitation Interventions in India: Gender Myopia and Implications for Gender Equality’, Indian Journal of Gender Studies, 26, 40–58.

[12] Massay, G., 2020. The struggles for land rights by rural women in sub-Saharan Africa: The case of Tanzania. African journal of economic and management studies, 11 (2), 271–283.

[13] Mengistu, B., 2012. ‘Empowering women and girls: How water, sanitation and hygiene deliver gender equality’, WaterAid. [Online] Available at: https://washmatters.wateraid.org/publications/empowering-women-and-girls-how-water-sanitation-and-hygiene-deliver-gender-equality [Accessed 19 May 2023].

[14] Ministry of Health and Social Welfare, 2008. National Guidelines for Implementation of Community Based Health Initiatives. Dar-es-Salaam: The United Republic of Tanzania.

[15] Moser, C., 1993. Gender Planning and Development: Theory, Practice and Training. London: Routledge.

[16] OVERDUE Mwanza City Team, 2022. Making sense of the official rules and social norms regulating sanitation in Mwanza, Tanzania. Video by OVERDUE Project prepared for the Development Studies Association Annual Conference. [Online] Available at: https://vimeo.com/720819174 [Accessed 19 May 2023].

[17] Rickard, K., 2022. ‘Enhancing Women’s Empowerment through Savings Groups’, in T. Redford, D. and Verhoef, G. (eds) Transforming Africa, Emerald Publishing Limited, 45–58.

[18] Rusca, M., et al., 2018. ‘Sanitation Justice?: The Multiple Dimensions of Urban Sanitation Inequalities’, in Water Justice. Cambridge University Press. pp. 210–225.

[19] Schmitt, M., Clatworthy, D., Ogello, T., & Sommer, M., 2018. Making the Case for a Female-Friendly Toilet. Water (Basel). 10(9), 1193.

[20] Truelove, Y., 2011. (Re-) Conceptualizing water inequality in Delhi, India through a feminist political ecology framework. Geoforum, 42(2), 143–152.

[21] UN, 2015. SDG Goal 5: Achieve gender equality and empower all women and girls. [Online] Available at: https://sdgs.un.org/goals/goal5 [Accessed 19 May 2023].

[22] UNICEF (2023) ‘Disability Inclusive WASH Practices: Including people with disabilities in UNICEF Water, Sanitation and Hygiene (WASH) Programming’, UNICEF. [Online] Available at: https://www.unicef.org/media/126126/file/Wash-and-disability-guidance-note-final.pdf [Accessed 17 May 2023].

[23] Van Aelst, K., 2014. Household decision-making and gender relations in Tanzania: literature and theory review. IOB Working Papers 2014.02, Universiteit Antwerpen, Institute of Development Policy (IOB).

[24] Vouhé, C. et al., 2021. Toilets are seats of gender equality: Gendered taboos surrounding sanitation deeply impact women and girls. Blog Post by OVERDUE Project. [Online] Available at: https://overduejustsanitation.net/?p=3994 [Accessed 18 May 2023].

Kwa taarifa zaidi wsiliana na:
Adriana Allen (a.allen@ucl.ac.uk),
Tim Ndezi (ccitanzania@gmail.com) au
Wilbard Kombe (kombewilbard18@gmail.com)